OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MGERA
S. L. P. 95 , SONGE - KILINDI

KUMB. NA.MGRSS/JI/13/2021 **Tarehe**.....

JINA LA MWANAFUNZI:.....
SHULE ATOKAYO.....

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MGERA WILAYA YA KILINDI MKOA WA TANGA MWAKA 2021.**

1.0. Nafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kuanza masomo ya sekondari (Kidato cha kwanza) katika Shule hii. Ni matumaini ya Shule na Taifa kwa ujumla kwamba utaitumikia vizuri nafasi hii. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021**

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 **SARE YA SHULE**

A. **WAVULANA**

i. Suruali mbili za rangi ya Kijivu zisizo na mapambo yoyote zaidi ya rinda mbili za mbele, mfuko mmoja wa nyuma na mifuko miwili ya pembeni. Pia isiwe ya kubana mwili (modo) na iwe ndefu ya kutosha
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto na yasiwe ya kubana mwili
iii. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu na viwe vya kufungwa kwa kamba na soksi nyeupe jozi mbili
iv. Sweta ya rangi ya kijivu
v. Tai ndefu ya kufunga shingoni rangi ya kijivu

B. **WASICHANA**

i. Sketi mbili rangi ya Kijivu mshono wa **RINDA BOX** na ziwe ndefu za kufikia kifundo cha mguu, ziwe za heshima na zisibane mwili
ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mifupi na mfuko mmoja upande wa kushoto na yasibane mwili
iii. Sweta rangi ya kijivu
iv. Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba na soksi nyeupe jozi mbili
v. Tai ndefu ya kufunga shingoni rangi ya kijivu

MUHIMU: Kwa wanaoshona **HIJABU** rangi ya hijabu ifanane na shati la shule na ishonwe kukidhi malengo ya vazi hilo na si vinginevyo

MICHEZO

Sare za michezo kwa wanafunzi wote zitakuwa

i. Track suti za bluu
ii. T- shirt ya bluu isiyokuwa na maandishi yoyote

VIFAA VYA DARASANI

i. Daftari aina ya counter book 9 isiyopungua Quire 2
ii. Begi la Shule na sio mfuko mwingine wowote
iii. Dictionary (Kamusi ya kingereza)
iv. Mathematica set (Mkebe wa mahesabu)

MUHIMU : Kwa wazazi wenye wanafunzi wanaotoka mbali wawasiliane na Uongozi wa Shule ili waelekezwe maeneo salama yanayofaa kuwapangishia watoto wao.

Pamoja na barua hii naambatanisha na nakala ya

i. Sheria za Shule (zisome na uzielewe
ii. Medical examination form : Ijazwe na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali (Songe) na kukabidhiwa kwa mkuu wa Shule siku ya kuripoti
iii. Fomu ya kukiri kwa mzazi na mwanafunzi ijazwe kikamilifu na kukabidhiwa kwa mkuu wa Shule siku ya kuripoti
iv. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa /Affidavit)

KARIBUNI SANA MGERA SEKONDARI

HEADMASTER
MGERA SECONDARY SCHOOL
KILINDI-TANGA

.....

FRANK KASANDA AMWORO
MKUU WA SHULE
0759345874/0752612474

1. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiw kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
g) Kuvaa mavazi ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

2. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, Kubeli nk.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza kuvuruga Amani na Usalama wa shule au watu
12. Kukataa adhabu
13. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI
SHULE YA SEKONDARI MGERA
S. L. P 95 – SONGE

FOMU YA MAELEZO BINAFSI

A. KUKUBALI KUJIUNGA *(ijazwe na mwanafunzi)*

Mimi ..... nakubali kupokea nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari ..... na naahidi kuitumia nafasi hiyo vizuri, pia naahidi kutekeleza maagizo na kufuata taratibu na sheria zote za shule.

Sahihi ya Mwanafunzi ..... *Tarehe* .....

B. MKATABA WA KUTOGOMA NA KUTOFANYA VURUGU SHULENI

(ijazwe na mwanafunzi)

Mimi ..... naelewa kuwa kufanya mgomo au vurugu shuleni ni kosa la jinai, hivyo naahidi kutoshiriki katika mgomo au kufanya fujo yoyote hapa shuleni.

Sahihi ya Mwanafunzi ..... *Tarehe* .....

C. **MAELEZO YA MZAZI AU MLEZI** *(Ijazwe na Mzazi au Mlezi)*

Mimi ..... ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi ..... Nakubali nafasi aliyopewa mwanangu kuendelea na masomo. Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule, naahidi kumsaidia mwanangu kwa kutimiza maagizo yaliyoagizwa katika fomu ya kujiunga. Nitaisaidia shule katika malezi ya mwanangu.

Sahihi ya mzazi / mlezi ..... *Tarehe* .....